Mwananchi Jumapili Agosti 31, 2025 Pg 1



# Mambo safi usafiri wa mwendokasi Mbagala -Morocco

HABARI UK6

CamScanner

Mwananchi Jumapili Agasti 31, 2025



USAFIRISHAJI

# Mwendokasi Mbagala kwenda hadi Morocco

Nasra Abdallah, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Wakati mabasi yaendayo haraka 'mwendokasi' kwa ajili ya Mbagala yakitarajiwa kuanza kutoa huduma kesho taarifa ya awali, sasa njia za safari zimeongezwa hususan 'ruti' ya Morocco.

Mbali ya hilo, idadi ya mabasi pia imeongezeka na kufikia 151.

Mabasi hayo yaliyokuwa yafanye safari kati ya Mbagala-Gerezani na Mbagala -Kivukoni, sasa yatakwenda pia Morocco, wilayani Kinondoni.

Vilevile, mabasi 52 yameongezwa na kufanya idadi ya yaliyowasili nchini hadi sasa kufikia 151.

Hayo yalielezwa juzi na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart), Dk Athuman Kihamia wakati wa kuyatoa mabasi hayo katika Bandari ya Dar es Salaam na kuyapeleka kwenye karakana iliyopo Mbagala Rangi Tatu.

Kazi ya kuyatoa mabasi hayo bandarini ilianza juzi, saa tatu usiku.

Mradi huo wa awamu ya pili kutekelezwa ukitanguliwa na ule wa Kimara ulioanza mwaka 2016, kampuni ya wazawa ya Mofat ndiyo imepewa mkataba wa miaka 12 wa kuuendesha ikitarajia kuingiza nchini mabasi 255. Idadi ya yaliyokwisha kufika ni 152.

**255**

**Ni jumla ya mabasi yanayotarajiwa kuingizwa nchini ya mwendokasi Mbagala.**

Hata hivyo, wakati mradi wa kwanza ulihitajika kuwa na mabasi 302, huu wa awamu ya pili unahitajika kuwa na jumla ya mabasi 755.

Ilielezwa ndiyo awamu yenye mabasi mengi kulinganisha na nyingine sita zitakazokuwapo katika miradi ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT).

Kwa mujibu wa Dk Kihamia, katika uletaji wa mabasi hayo awamu ya kwanza 99 yalifika nchini Agosti 5, huku 52 yakiingizwa Agosti 26. Mengine 153 yanatarajiwa kuletwa katikati ya Oktoba na kufanya idadi kufika 255.

Dk Kihamia alisema tofauti na awali, mabasi hayo sasa yatatoa huduma Mbagala kwenda Gerezani, Mbagala kwenda Kivukoni na Mbagala kwenda Morocco.

"Mabasi haya 151 yatatoa huduma katika barabara hizo na tutayaelekeza kulingana na mahitaji ya usafiri kwa wakati husika, huenda eneo fulani likawa na uhitaji zaidi tukaachia magari 50 kwa wakati mmoja, hususani asabuhi watu wakienda kazini na jioni wakirejea majumbani. Kwa kuwa tuna mfumo wa kisasa wa kuongozea magari utakuwa ukituonyesha hayo yote," alisema.

Amesema magari yote yakishawasili yatakwenda kutatua changamoto ya usafiri.

Dk Kihamia akizungumzia madereva, alisema wamepata mafunzo ya uhakika ya uendeshaji na ana imani hakutakuwa na ajali zinazosababishwa na uzembe kutoka kwao.

"Hata hivyo, ili hili lifanikiwe ni vema wananchi kuacha kutumia barabara za magari hayo kwa kuwa yanaenda haraka na yatakuwa mengi barabarani, hivyo ajali zinaweza kuwa nyingi zaidi kama hawatakuwa makini. Ni vema tukayalinda na kuyatunza mabasi haya, lakini na sisi tukajilinda na ajali za kujitakia wenyewe,"alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mofat, Muhammad Abdallah Kassim, alishukuru namna Serikali ilivyoshirikiana nao kwa karibu kuhakikisha mabasi hayo yanatoka bandarini.

"Kwa kweli tunaishukuru Serikali ilivyokuwa bega kwa bega na sisi kuhakikisha tunayatoa mabasi haya ndani ya muda mfupi, kwani ingekuwa siyo ushirikiano wao huenda ingechukua muda zaidi ukizingatia yapo mengi," alisema.

Alisema wamejipanga vilivyo katika utoaji huduma, akieleza ana imani abiria watazifurahia.

Kassim alisema abiria watakaopanda mabasi hayo ukiacha kuwa yana viyoyozi, watapata huduma ya mtandao bure.

"Tumeshaongea na kampuni ya mtandao (anaitaja) kuhusu kufunga mtandao wa bure kwenye mabasi yetu, hivyo mtu ukipanda humu hata kama hauna bando utaweza kuperuzi kama kawaida," alisema.

Kassim alisema kwa watakaoishiwa chaji wataweza kuchaji ndani ya mabasi hayo.

Vilevile, katika kudhibiti matukio ya wizi ndani ya mabasi kumefungwa kamera, lengo likiwa kuhakikisha usalama.

"Gari zetu ni za kisasa na zimezingatia matakwa ya usafiri wa kimataifa. Tuna imani watakaopanda watafurahi, lengo ni kuona hata aliye na usafiri wake binafsi anauacha nyumbani na kutumia huu," alisema.



Sehemu ya mabasi ya mwendokasi yakiwa kwenye Kituo cha Mbagala Rangi Tatu baada ya kuwasili kutoka bandarini yalikokuwa yamehifadhiwa.

CamScanner

Mwananchi Jumapili Agosti 31, 2025 Pg 4



Bajaji ya kubeba abiria ikipita katika Barabara ya Mabibo Relini huku ikiwa imebeba mzigo wa kitanda pamoja na godoro,- jambo ambalo ni kunyume na sheria za usafiri huo barabarani. **Picha na Paulo Mungo-TASUBA**

CamScanner